



Katika kukusanya na kutumia maelezo ya kibinafsi, tunataka kubainisha kile tunachofanya na kuhakikisha unaelewa jinsi tunavyoyatumia.

1. Kwa nini tunakusanya data?

Mashabiki wanaweza kutangamana na Manchester City na pia City Football Group kwa njia kadhaa ikiwemo: kuhudhuria mechi, kutembelea tovuti yetu rasmi, kutangamana kwenye mitandao ya kijamii, kutangamana kwenye vifaa tamba, au kushiriki katika miradi yetu ya jamii.

Utangamano huu unazalisha maelezo kuhusu mashabiki wetu ni nani na wanachotaka. Maelezo haya yanaweza kutusaidia kuelewa ni nini fanisi, kuboresha bidhaa zetu na kuhakikisha tunatimiza matarajio ya mtu binafsi kama shabiki.

Aidha, kuna manufaa yanayoongezeka wakati shabiki anapojisajili na Manchester City:

- Habari za kipekee zinajumuishwa katika majarida yetu ya barua pepe
- Mashindano kabambe na tuzo zinazopeanwa
- Ufikiaji maudhui muhimu na yaliyobinafsishwa kupitia jukwaa letu la Cityzens
- Ushiriki katika tafiti za kutusaidia kuboresha Klabu
- Kusaidia Huduma kwa Mashabiki kuweza kujibu maswali yoyote ambayo huenda ukawa nayo

Manchester City ndio 'mdhibiti' data wa maelezo unayotoa na hatutawahi kuuza data zako.

2. Tunakusanya data zipi?

Unapojisajili na Manchester City, tunaunda ukurasa wa wasifu ili kuonyesha ni maelezo gani ya kibinafsi ambayo umetupatia, ambayo unaweza kuhariri unavyotaka na unapotaka. Baada ya muda, tutaangazia data zaidi ambazo huenda zikakuvutia au zikawa muhimu kwako, kama vile historia ya miamala yako na maudhui ya mtandaoni ambayo huenda ukafurahia.

- **Jina la Kwanza na Jina la Mwisho:** Tunaomba jina lako ili tuweze kukupa huduma ya kibinafsi na fanisi zaidi. Timu yetu ya Huduma kwa Mashabiki itajua wewe ni nani na kufikia maelezo yako mara moja.
- **Tarehe ya Kuzaliwa na Jinsia:** Maelezo haya ni muhimu ili kuelewa jinsi mashabiki wetu wanavyoendelea na kwa ajili ya usalama. Pia yanatusaidia kukupa mapendekezo bora zaidi na yanayokufaa zaidi. Pia tutakutumia ujumbe wa siku ya kuzaliwa ikiwa umechagua kupokea ujumbe huu.
- **Anwani na Eneo:** Hii hasa ni muhimu tunapohitaji kuwasilisha bidhaa kwako. Maelezo haya pia yatueleza ni wapi mashabiki wetu wapo nchini Uingereza na kote ulimwenguni. Tena, yanatusaidia kukupa maelezo abayo yanakufaa zaidi.

Mara kwa mara huenda tukapata maelezo ya ziada kukuhusu wewe kutoka kwa vyanzo vingine vya data ambavyo ni vya kuaminika ili kuweza kuelewa mengi zaidi kuhusu ni nani anayetumia bidhaa na huduma zetu. Hii inatusaidia kujua mengi zaidi kuhusu mtindo wa maisha yako na mambo yanayokuvutia na tunaweza kutumia maelezo haya, pamoja na kuki na teknolojia sawia kama vile Matangazo kulingana na Tabia za Mtandaoni (Online Behavioural Advertising), ili kukupa ofa na maudhui yanayokufaa zaidi. Sera yetu ya Kuki ina maelezo zaidi kuhusu hili.

Unaweza kujiondoa wakati wowote na unaweza kuchagua unachotaka kupokea katika kituo chako cha mapendeleo kinachofikiwa kupitia tovuti au barua pepe.

3. Tunafanya nini na data tunazokusanya?

Manchester City itatumia maelezo tunayokusanya kuhusu watu binafsi kwa njia zifuatazo:

- Kusaidia kufuatilia, kuchambua na kuboresha maudhui na bidhaa tunazotoa
- Kuwawezesha mashabiki kushiriki katika vipengele tangamanifu za bidhaa na huduma zetu za kidijitali
- Kuwapa mashabiki huduma iliyobinafsishwa zaidi, kwa mfano kwa kufanya mapendekezo ya maudhui na bidhaa
- Kuwasaidia mashabiki vyema zaidi kuhusu maswali, malalamishi au maombi kupitia mbinu zetu za mtandaoni, simu na barua
- Kutuwezesha kuwasilisha bidhaa na huduma ambazo shabiki ameomba, kama vile tikiti na bidhaa

Pia tumejitahidi kutengeneza Sheria za Matumizi na Sera ya Faragha, ambazo ni wazi na rahisi kusoma, zinazoeleza kwa kina hata zaidi kile ambacho tunafanya na data zako.

Wakati wowote ukiamini kwamba maelezo tuliyo nayo kukuhusu wewe si sahihi, unaweza kuomba kutazama maelezo haya na uyasahihishe au uyafute. Tafadhali wasiliana na timu yetu ya Huduma kwa Mashabiki [hapa](#)

Ikiwa ungependa kuibua lalamishi kuhusu jinsi ambavyo tumeshughulikia data zako za kibinafsi, unaweza kuwasiliana na Ofisa wetu wa Ulinzi wa Data, Simon Cliff kupitia DPO@cityfootball.com.

Ikiwa haujaridhishwa na jibu letu au unaamini kwamba hatusindikia data zako za kibinafsi kulingana na sheria, unaweza kuweza kuwasilisha lalamishi kwenye Ofisi ya Kamishina wa Taarifa (Information Commissioner's Office, "ICO").

Maelezo ya mawasiliano ya ICO ni:

The Information Commissioner

Wycliffe House

Water Lane,

Wilmslow

SK9 5AF